

JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UPIMAJI WA HARAKA (COVID-19 RAPID TESTING)
KWENYE VIWANJA VYA NDEGE KWA WASAFIRI WANAOKWENDA NJE YA NCHI

Ndugu Wananchi,

Kufuatia ongezeko la visa vipya vya maambukizi, nchi zimeweka taratibu mbalimbali kwa wasafiri kuingia na kutoka ili kudhibiti kusambaa kwa maambukizi ya COVID-19. Taratibu hizi ni pamoja na kuweka sharti la kupima COVID-19 ili kupunguza au kuzuia kuingia kwa ugonjwa huu katika nchi hizo.

Ndugu Wananchi,

Ninapenda kuwafahamisha kuwa wasafiri wote wanaoishia nchi za Marekani, Nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu, baadhi ya nchi za Ulaya na India watatakiwa kufanyiwa kipimo cha haraka (*COVID-19 Rapid Antigen Test*) kabla ya kuondoka. Ili kudhibiti maambukizi wasafiri wanatakiwa;

- a) Kuwa na cheti halali cha kipimo cha COVID-19 RT-PCR
- b) Kufanya kipimo cha haraka (*COVID-19 Rapid Antigen Test*) Uwanja wa Ndege ndani ya masaa 6 kabla ya kusafiri kwa wasafiri wanaokwenda Marekani, India na baadhi ya nchi za Ulaya.
- c) Kufanya kipimo cha haraka cha PCR (*COVID-19 Rapid PCR test*) kama unaenda nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu, au kupitia Dubai.
- d) Wasafiri wote wanaunganisha usafiri wa ndege kupitia Tanzania wanapaswa kufanya kipimo cha haraka (*COVID-19 Rapid Antigen Test*) katika uwanja wa ndege ndani ya masaa 6 kabla ya kusafiri.
- e) Kuwa na cheti halali cha chanjo ya COVID-19

Ndugu Wananchi,

Ninapenda kuwasihi na kuwasisitiza kuendelea kuchukua hatua za kujikinga na ugonjwa wa COVID-19 kama vile kuchanja, kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka, kuvaa barakoa na kuepuka misongamano. Wizara itaendelea kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha inawakinga wananchi wake dhidi ya ugonjwa wa COVID-19.

Utekelezaji wa baadhi ya maagizo haya ulishatolewa taarifa kwa umma siku zilizopita na kwa yale masharti mapya, unaanza tarehe 25 Disemba 2021.

Imetolewa na;

Prof. Abel N. Makubi
KATIBU MKUU (AFYA)

24 Disemba 2021